

**Kifanyiwa Ukaguzi wa
Fupanyonga na Upimaji
wa Saratani ya Mlango
wa Kizazi**




Kujiandaa kwa Ukaguzi wa Fupanyonga

- Muuguzi atakuuliza kuhusu afya yako.
- Utaingia kwenye chumba cha ukaguzi. Utapewa gauni ya karatasi uvae na shuka ujifunike.
- Utalala chini kwenye meza shuka ikiwa imefunika miguu na tumbo lako. Utaweka magoti yako kando kandi na uweke miguu yako katika vishikizi vinavyoitwa vikuku.

Kufanyiwa Ukaguzi

- Daktari au muuguzi ataangalia sehemu yako ya uke aone kama una dalili zozote za maambukizo au matatizo mengine.
- Muuguzi au daktari atatelezesha kipande chembamba cha plastiki au chuma kinachofanana na mdomo wa bata ndani ya uke wako kukagua ndani yake.
- Wakati wa upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi, muuguzi au daktari atatumia brashi ndogo kuchukua seli chache kutoka kwa mlango wako wa kizazi (mlango wa uterasi). Maabara itakagua seli hizi kwa saratani au matatizo mengine. Ikiwa saratani itagunduliwa mapema, itakuwa rahisi kutibu.



- 
- Baada ya upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi, muuguzi au daktari atakagua fuko zako, ovari, na uterasi (tumbo la uzazi) kwa kuweka vidole viwili akiwa amevaa glavu ndani ya uke wako. Akitumia mkono wake mwingine, atatafuta uvimbe au ulaini kutoka upande wa nje. Hii itachukua dakika chache tu.
 - Ukaguzi umekamilika na unaweza kuvaa nguo.
 - Hakikisha unauliza maswali yoyote uliyo nayo kabla ya muuguzi au daktari kuondoka kutoka kwa chumba.

Matokeo mengi ya upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi huwa ya kawaida.

Dakitari au kliniki itawasiliana na wewe ikiwa matokeo yako sio ya kawaida.

Mpigie daktari wa familia yako au kliniki ya kimatibabu iliyo karibu simu LEO kwa miadi ya upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi.

Miadi yangu ya upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi:

Tarehe: _____

Saa: _____

Wapi: _____

Simu: _____



Imechukuliwa na kutafsiriwa kutoka Chapisho la NIH Na. 99-3416.
Fedha za utengenezaji wa kijitabu hiki: NCI AANCART CA86322.
Kijitabu hiki hakipatikani kwa sasa kwa usambazaji wa jumla.

